

SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Simu: 2133990
Telegramu: Railways
Nukushi: 2133428



Ofisi ya Uhusiano
S.L.P 70364
Dar es Salaam

TAARIFA KWA UMMA

KUKANUSHA TAARIFA ZA UONGO ZILIZOCHAPISHWA NA GAZETI LA TANZANIA MPYA

Dar es Salaam, Novemba 4, 2019:

Shirika la Reli Tanzania (TRC) hivi karibuni limebaini taarifa za upotoshaji umma zilizochapishwa na Gazeti la TANZANIA MPYA likiwa na kichwa cha Habari "**TRC YANUKA RUSHWA**" na kufuatiwa na habari nyingine isemayo, "**TBS, TRC WINGU ZITO**".

TRC inapenda kuutaarifu umma kuwa habari hii ipuuzwe kwani ni ya uongo, uzushi na iliyosheheni malengo yasiyoleweka nia yake kwa Shirika na Serikali kwa ujumla kwani hata wahariri wa gazeti walipoitwa na Msajili wa Magazeti kuthibitisha habari hiyo walikosa vielelezo na kuomba msamaha.

Wakati Msajili wa Magazeti akiendelea na hatua zake za kisheria dhidi ya uongo huo uliopitiliza, TRC inaendelea kuwahakikishia Watanzania kuwa Uongozi wa Shirika uko makini na utaendelea kusimamia mali na maslahi ya Shirika na Serikali kwa weledi, kujituma, kujitoa na kuzingatia sheria za nchi.

Imeandaliwa na:

Jamila Mbarouk

Mkuu wa Kitengo Uhusiano TRC

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'JM'.